**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI-TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
**Mkuu wa Shule:** 0682 498556
**Makamu Mkuu wa Shule:** 0787 187531
**Matron:** 0688663461
**Patron:** 0625919983

**Shule ya Sekondari Kiteto**
**S.L.P 86, Kibaya-Kiteto**
**Tarehe ......................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITETO HALMASHAURI YA WILAYA KITETO MKOA WA MANYARA MWAKA 2024/2025.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Kiteto ipo umbali wa Kilometa mbili (2) Kaskazini-Mashariki mwa Mji wa kibaya Usafiri wa pikipiki (bodaboda) na Bajaji kutoka mjini kibaya unapatikana katika kituo cha mabasi kibaya. Nauli ni Shilingi elfu mbili (2000/=) kwa pikipiki na Shilingi elfu tatu (3000/=) kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .............

**A. MAHITAJI YA SHULE**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule

- Akaunti **Na. 50101100015 KITETO SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT** Benki ya NMB

Aidha ulete **Bank Pay in Slip (BPS)** ikiwa inaonesha majina kamili ya mwanafunzi. ***Fedha taslim haipokelewi shuleni.***

**B. MAHITAJI YA DARASANI**

i) Madaftari makubwa ya masomo nane kwa tahasusi za sayansi na madaftari saba kwa tahasusi za sanaa (counter book quire 3)

ii) Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi (fx991)

iii) Vitabu kulingana na Tahasusi yake ***(hasa vitabu vya TIE), na vilivyoorodheshwa kwenye list angalau kisipungue kimoja kwa kila somo*** .

iv) Mathematical set moja

v) Dissecting kit kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.

vi) Begi la kubebea madaftari

vii) **Ream = A4 moja na Rulled moja kwa muhula**

**Mahitaji mengine muhimu**

- Tochi (kwa matumizi binafsi wakati umeme umekatika)
- Pasi ya mkaa (**pasi ya umeme hairuhusiwi**).

**C. SARE NA MAHITAJI MENGINE MUHIMU 1. WASICHANA**

- Sketi ya kijivu **Mpauko (grey)** Mbili. Mshono ni marinda nane kama inavyoonekana hapo chini.

**Muhimu**: urefu wa sketi; **ifike chini kwenye kifundo cha mguu, isiwe ya kubana na iwe ya kitambaa kizito.**



- Shati mbili au zaidi nyeupe za mikono mirefu (aje akiwa amevaa sare ya shule).
- Tai ndefu ya kijivu.
- Sweta la kijivu halisi (original) kama inavyoonekana kwenye picha hapa chini.



- T-Shirt rangi ya bluu bahari au unaweza kuipata shuleni kwa Tsh. 12,000/-



- Rangi ya hijabu (juba) ni nyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu (isiyo na urembo).
- Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi (na sio simple). **Soksi ndefu** nyeupe jozi mbili au zaidi.
- Nguo za kushindia (shamba dress): sketi nyeusi mbili mshono wa rinda boksi (iwe ndefu ivuke vifundo vya miguu) na vijuba vyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu (visivyo na urembo)
- Sare za michezo shuleni:Track suit ya **bluu bahari** na raba nyeupe.
- Shuka mbili za **bluu bahari**, blanket 1, foronya ya godoro 1 na chandarua (light blue).
- Sanduku linalofunga vizuri (la chuma) na siyo safari begi
- Godoro  (futi 2 ½ x 6)

***2.* WAVULANA**

- Suruali ya **kijivu Mpauko (grey)** mbili au zaidi, mshono; suruali iwe na **marinda** mawili (celebration), **pindo chini (turn up)** na upana wa chini miguuni (**nchi 16**) ***MUHIMU mshono wa jinsi/modo hauruhusiwi.***

***NB: Rangi halisi ya suruali inafanana sawa na rangi ya sketi kwa wasichana. (Tizama picha hapo juu).***

- Shati nyeupe mbili au zaidi za mikono mirefu.
- Tai ndefu rangi ya **kijivu**.
- Sweta la kijivu halisi (Original)
- T-Shirt rangi ya bluu bahari au unaweza kuipata shuleni kwa Tsh. 12,000/-



- Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (**sio buti**) na soksi nyeusi jozi zaidi ya moja.
- Nguo za kushindia (shamba dress); suruali nyeusi mbili, mshono ufanane na sare za darasani.
- Jezi: bukta, T-shirt rangi ya bluu yenye shingo ya duara isiyo na maandishi, na viatu vya michezo.
- Shuka mbili za **bluu bahari**, blanket 1, foronya ya godoro 1 na chandarua (light blue).
- Sanduku linalofunga vizuri (la chuma) siyo safari begi
- Track suit ya bluu bahari
- Godoro (futi 2 ½ x 6 )

ZINGATIA: ***Nguo ambazo sio sare ya shule haziruhusiwi kabisa, ukaguzi utafanyika mara baada ya kuwasili shuleni na endapo utakutwa nazo zitachomwa.***

## *D.* VIFAA VYA USAFI SHULENI

- Ndoo kubwa mbili (lita 20) moja utakabidhi na nyingine ya matumizi binafsi.
- Sahani, kikombe, kijiko (vyombo vya plastiki haviruhusiwi)
- Ufagio wa chelewa (mmoja)
- Jembe na mpini (kwa tahasusi za PCB, HKL, HGK, HGLi na HGFa), beleshi (kwa tahasusi ya CBG).
- Squeezer 1, soft broom 1 na brash ya kusugulia sinki la choo.

  ***NB. Vifaa tajwa vinapatikana kiteto mjini.***

## *E.* SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu ya Mwaka 1978 na inazingatia miongozo inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Aidha, wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia haya yafuatayo;

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kutambua kuwa yuko hapa kwa ajili ya KUSOMA kwa faida yake, familia yake na Taifa lake kwa ujumla. Kwa sababu hiyo chochote kilichopo nje ya jukumu hili hakina nafasi katika shule hii.

**Mahudhurio**

- Kuwahi shuleni ni wajibu wa kila mwanafunzi hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa na kuendelea kuwepo shuleni kila siku.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa. Vipindi vya kazi za mikono pamoja na kazi za mikono ni sehemu ya masomo.
- Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikusanyiko halali yote ya shule kama vile mstarini, usafi, baraza la shule, ibada, midahalo (debates), n.k
- Ni lazima kutimiza kwa makini mahudhurio ya maandalio ya jioni (evening preparation).
- Kila mwanafunzi anawajibika kuwahi kula chakula kwa wakati uliopangwa. Ni marufuku kuwahi kuchukua chakula kabla ya wengine. Kama kuna tatizo lolote liripotiwe kwa mwalimu wa zamu au wa chakula.

**Sare za shule**

- Wanafunzi wote ni lazima kuvaa sare za shule muda wote wa darasani na wanapotoka nje ya shule.
- Mwanafunzi lazima ajiweke katika hali ya usafi, kimwili na kimavazi. Nguo zote atakazovaa mwanafunzi lazima zikubaliwe na uongozi wa shule pale anaporipoti mwanafunzi shuleni tu.
- Nguo za michezo, shamba dress, track suit zitavaliwa kulingana na ratiba iliyopangwa.

**Heshima na utii**

- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote alipo, ndani na nje ya mipaka ya shule.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kutii kengele, kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wote, viranja wa shule na jumuiya nzima ya shule.
- Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kumpokea na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au aingiapo shuleni au darasani.
- Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, nembo ya Taifa na picha za viongozi wa serikali.

**Sehemu muhimu za kujifunzia.**

- Madarasa, maabara na maktaba ni sehemu za masomo hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele, kuzomea, kupiga gumzo au kuzurura ndani ya sehemu hizo.
- Ni marufuku kuingia kwenye maabara bila kibali cha mwalimu husika.
- Ni lazima kila mwanafunzi atumie maktaba kufuatana na sheria za maktaba.

**Afya;**

i. Kila mwanafunzi ahakikishe anakuwa na ***BIMA YA AFYA YA TAIFA (NHIF)*** au aje na mchango wa shilngi 50,400/= kwa ajili ya bima ya NHIF kwa wasio na bima.
ii. Kila mwanafunzi lazima ajiweke katika hali nzuri ya kiafya ili aweze kuyamudu masomo yake vyema.
iii. Endapo mwanafunzi ataugua ataomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu mshauri wa wanafunzi.
iv. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule tu. iii) Gharama za matibabu zilizo nje ya bima zitagharamiwa na mzazi/mlezi wako. iv) Mwanafunzi hatakiwi kuchafua mazingira ya shule kwa namna yoyote, mfano; kutupa taka ovyo.

v. Mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake ikiwa ni pamoja na kukata kucha, kunyoa nywele na ndevu, kutandika kitanda, kuoga na kupiga mswaki, kupanga vitu vyake vizuri bwenini, n.k

***NB: Wasichana hawaruhusiwi kusuka***

**Mipaka ya shule**

- Mwanafunzi yeyote atakayetoka nje ya mipaka ya shule lazima awe amepata kibali cha mwalimu wa zamu na awe amevaa sare ya shule.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo; vilabu vya pombe, majumba ya starehe, na nyumba za kufikia wageni (guest house).

**Vifaa na mali za shule.**

- Ni marufuku kuandika au kuweka alama/chata katika kuta, milango, meza au dawati au kitu ambacho ni mali ya shule.
- Uharibifu wowote au upotevu wa kitu chochote cha shule lazima ufidiwe.
- Mali zote za shule utakazokabidhiwa utalazimika kuzirudisha zikiwa katika hali nzuri, vinginevyo utalipia uharibifu.

**F. MAKOSA AMBAYO YANAWEZE KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI**

(i) Wizi.
(ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xii) Kutembelea nyumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi/chipu ya simu/charger ya simu/memory card katika mazingira ya shule. Endapo itakamatwa kwanza; itaharibiwa hadharani na hatua nyingine kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule. (xiv) Kudharau Bendera yaTaifa/Wimbo wa Taifa/Nembo ya Taifa/Wimbo wa shule (xv) Kufanya jambo lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
(xvii) Utoro wa shule, mahudhurio mabovu darasani au kukosa kufanya mitihani/majaribio/mazoezi bila taarifa au kibali maalum cha mkuu wa shule.
(xviii) Kukaa bwenini wakati wa vipindi bila kibali cha mkuu wa shule.
(xix) Kuingia bweni la jinsi tofauti.
(xx) Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa au kibali.
(xxi) Kuingia na chakula cha aina yoyote bwenini.
(xxii) Kugoma au kukataa adhabu kwa makusudi.

## *G.* MAELEKEZO

Fomu zifuatazo zijazwe na uje nazo shuleni zikiwa kamili; -
Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi na mzazi.

- **Nakala ya cheti cha kuzaliwa.**
- **Nakala ya Result Slip ya kidato cha nne.**
- **Fomu ya matibabu (medical examination form).**

Muhimu: ***Siku ya kutembelea wanafunzi ni jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 4:00asubuhi - 10:30 jioni tu ili kuepuka usumbufu usio wa lazima labda kama imeelekezwa vinginevyo. Pia mwanafunzi asipewe mchango wowote wa shule bila maelekezo kutoka kwa mkuu wa shule. Aidha mawasiliano ya simu kati ya mzazi na mwanafunzi ni mara moja kwa mwezi.***

*KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KITETO!*

**KIMARO J.**

**MKUU WA SHULE.**

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI NA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

ANUANI YAKO …………………….

S. L. P …………………

MKUU WA SHULE,

KITETO SEKONDARI,

S. L. P 86,

**KIBAYA – KITETO.**

Mimi ……………………………………………………………….. (majina rasmi kwa herufi kubwa kama yanavyoonekana kwenye vyeti) nimesoma na kuelewa vizuri maagizo na masharti ya kujiunga kidato cha tano hadi cha sita kwa mwaka 2024/2025.

Ninaahidi kuwa nitayatimiza yote yaliyoandikwa pamoja na kanuni na taratibu nyingine nitakazopewa nifikapo/niwapo shuleni.

Ninaomba nipokelewe shuleni, na iwapo nitakwenda kinyume cha masharti, kanuni na taratibu hizo nitakuwa tayari kupokea adhabu nitakazopewa kulingana na makosa nitakayokuwa nimeyatenda.

**Saini yangu ………………………**

**Tarehe ………………………….**

***Zingatia;*** sehemu ya chini ijazwe mzazi/mlezi.

Mimi mzazi/mlezi ………………………………………………………………..

Nimesoma kwa makini maelezo na kanuni, sheria na taratibu zote za shule

***Nipo/sipo*** tayari kushirikiana na shule wakati wote wa masomo kuhusu malezi ya kijana wangu.

**Saini ya mzazi/mlezi ………………………………    Tarehe ………………**

**Simu ………………………….**

Mawasiliano kuhusu taarifa na mienendo ya mwanangu itumike simu ya mkononi ………………………..

Endapo kuna dharura aarifiwe ndugu wa karibu aitwaye ……………………………………………..

ambaye ni (uhusiano) ………………………………………………simu ya mkononi ……………………

1. Ikumbukwe kwamba wakati wa likizo wanafunzi wanasafiri kurudi kwa wazazi au walezi na si vinginevyo.
2. Mwanafunzi aje na picha nne za wazazi au walezi wa mwanafunzi wanaoweza kuja kumtembelea au kwa wito na namba zao za simu.

KITETO DISTRICT COUNCIL KITETO SECONDARY SCHOOL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From: Kiteto Secondary School,
P. O. Box 86, Kibaya – Kiteto.
Date: ……………………………

Medical Officer,
…………………………………..
P. O. Box ……………………….
……………………………………

Full Name: ………………………………………………………………………………...
Please examine the above named student to her fitness for entrance to this school in form five year 2024.

- Blood current …………………………………………………….………..
- Stool …………………………………………………………………………….
- Urinal analysis ……………………………………………………………….
- T.B test ……………………………………………………………………………
- Syphilis…………………………………………………………………………….
- Ears………………………………………………………………………………
- Chest ………………………………………………………………………………
- Spleen ……………………………………………………………………………..
- Eyes test……………………………………………………………………………
- Abdomen test…………………………………………………………………………

(**Check course of pregnancy**)

Additional information e.g. physical defects or permanent infection such as family chronic diseases etc..
…………………………………………………………………………………….......................
...........................................................................................................................................................
...................................................................................................………………………………………
……………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**
(**To be completed by medical officer**).
I have examine the above named and considered that she is fit/unfit for enrolment to the school above.

Name …………………………………… Signature ……………………. Date…………….

Station …………………………………… Designation …………………………………….

Official Stamp

NB: At the time of examination please treat the individual for an illness you note.

**KITETO SECONDARY SCHOOL**
**ADVANCED LEVEL – LIST OF BOOKS**

## 1. HISTORY

- Essential in Advanced Level History I, by Salehe Yasini
- Essential in Advanced Level History II, by Salehe Yasini
- Contemporary History for Advanced Level History I&II, by Shibital

## 2. GEOGRAPHY

- Pritchard M, John (1971) Practical Geography for Africa.
- PT. Msabila (2007) A Comprehensive Approach to Physical Geography for secondary schools
- Msabila, DT (2000) An Integrated Focal Regional Study on Human and Economic Geography

## 3. KISWAHLI - 01

- Nadharia ya Lugha kidato cha 5 na 6 – Mwandishi Jubeck .A. Masebo
- Nadharia ya Lugha kidato cha 5 na 6 na Elimu ya Juu – Masuko C. Saluhaya
- Jikumbushe Kiswahili – 01 kidato cha 5 na 6 – Maswali na Majibu

### KISWAHILI – 02

- Tahakiki ya Kiswahili shule za sekondari kidato cha 5 na 6 – Kilargi .E. Lucas
- Fasihi kidato cha 5 na 6 – TIE (Taasisi ya Elimu Tanzania)
- Jikumbushe Kiswahili 2 kidato cha 5 na 6 – Maswali na Majibu.

## 4. ENGLISH LANGUAGE

- Advanced Level English Language Structure & Stylistics – A Practical Approach – Sichlous Asheli
- English for Advanced Secondary Schools – Student's Book Five – Tanzania Institute of Education (TIE)
- Language Two – by Kashen, S (1982)
- A Couse Book on Translation – by Baker, M (1992)
- Becoming a Translator; An Introduction to Theory and Practice of Translation – by Robinson, D (2003)

## 5. PHYSICS

- Advanced Level Physics 7th Edition by Michael Nelicon
- A-Level Physics 4th Edition by Roger Muncaster
- Principles of Physics XI by S. Chand
- Mastering Physics by Odas, Chades & Massey Massey
- Physics Text Book for class XII (Part I and II) by National Council of Educational Research and Training
- Advanced Physics Text Book by Tom Duncan, 5th Edition
- Understanding Physics volume 1 – 3 by Isaac Asimor, 3rd Edition
- New A – Level Mechanic Book 2 by Elias Kihombo

## 6. CHEMISTRY

- Freenmentle M. Chemistry in Action. Macmillan Education Ltd. 3rd edition
- Mzumbe Book Project : Physical Chemistry
- Arms & Patrick – Advanced Chemistry
- Conceptual Chemistry (Chand's) for class XII (Dr. S. K. Jain)
- Conceptual Chemistry (Chand's) for class XI (Dr. S.K. Jain)
- Ngaiza Series of Advanced Chemistry
  (General Chemistry, Physical Chemistry, Organic Chemistry, In Organic Chemistry, Environmental & Soil Chemistry).

## 7. BIOLOGY

- Biology for Advanced Level (TIE) Form Five and Form Six
- Biological Science (B.S) D.J Taylor, N.P.O Green and G.W Stout
- New Understanding Biology Advanced Level 4th edition
- Modern ABC Biology Volume 1 and 2
- Dissecting Kit (PCB&CBG) Ni lazima.
- Robert M.B – New Biology a functional approach 4th edition
- S. O. Loeje – Certificate Practical Biology
- C. Adavanced Biology – Principles and Application.

## 8. GENERAL STUDIES

- General Studies for Secondary Schools – by Mbalase, R.
  General Studies – by SETA
- Understanding General Studies for Advanced Level – by Jeanes B, & Sospeter M, D.

***Note; Knowledge is acquired through books but skills is obtained by practice, Bring with you at least one book for each subject from the list above.***